

## **Afrikan Entrepreneurs – Successful and Responsible**

### **Episode 9**

**Title: “Beading for a better life - Mathapelo Ngaka from South Afrika”**

**Author: Leonie March**

**Editors: Katrin Ogunsade / Adrian Kriesch**

**Proofreading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kiswaheli:Eric Ponda**

### **Characters (O-Töne, Clips) / Narrators**

	Women	Men	Age	Language
Intro/Outro		x	Unimportant	
Narrator	X		Unimportant	
Mathapelo Ngaka (clip)	X		Mid 30s	English
Joan Krupp (clip)	X		Mid 40s	English

### **Pronunciation [as it would be in english]:**

Mathapelo Ngaka: Matapelo Ngaka

Kayelitsha (pronounced as written)

isiXhosa (pronounced: izi'khoza)

Siziwe Lumkwana (pronounced as written)

## **Intro:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya Learning By Ear Noa Bongo Jenga maisha yako, tukiwaangazia wajasiriamali barani Afrika ambao wamefaulu na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kubadilisha maisha miongoni mwa jamii wanamoishi. Katika kipindi cha leo tunafunga safari hadi mjini Cape Town nchini Afrika Kusini kukutana na Mathapelo Ngaka ambaye amefaulu kuanzisha shirika lisilozingatia kupata Faida la “Monkeybiz”.

### ***1. Sound: Kayelitsha in front of Mathapelo’s house***

#### ***2. Narrator:***

Kayelitsha (pronounced as written). Ni eneo lililojaa takataka za vyuma kuu kuu, vumbi na nyumba ndogo zilizojengwa kwa matofali. Hapa ni sehemu inayoishi watu maskini ikizungukwa na mitaa ya watu matajiri mjini Cape Town nchini Afrika Kusini. Wakati wa enzi ya utawala wa ubaguzi wa rangu, ubaguzi wa rangi, na wa kisiasa, baina ya Weusi na waeupe lilikuwa jambo la kawaida hasa katika eneo hili. Wakati huo, kijiji hiki cha Kayelitsha kilikuwa miongoni mwa vijiji vilivyotengewa Wa-Afrika nchini Afrika Kusini. Na hapa ndipo hadithi yetu inapoanzaia.

#### ***3. Mathapelo:***

“Jina langu ni Mathapeleo, nina Umri wa miaka 36 na nimekuwa nikiishi katika mabanda haya kwa miaka mingi sana.. mingi tu. Kama ujuavyo wakati wa baridi mabanda haya yana ubaridi sana, kukinyesha yanavuja, maisha ni magumu san katika mabanda haya.”

#### **4. Narrator:**

Ni matatizo na Umaskini yaliyomfanya Mathapelo na familia yake kuja kuishi katika sehemu hizi za mashambani mjini Cape Town. Mamake alijitahidi licha ya hali ngumu ya maisha kuwalea watoto wake 5 baada ya Mumewe kuaga. Na kumbu kumbu ya maisha hayo magumu bado imemganda Mathapelo. Hivi leo anamtembelea Mamake katika kijiji hicho cha Kayelitsha ambako anaishi na Mumewe na watoto wao wawili. Si mbali sana, ni hatua chache tu kutoka nyumbani kwake. Na sio kwamba kina mama hawa wawili wanakutana tu kwa kikombe cha chai bali kushauriana kuhusu mipango ya kuanzisha biashara.

#### **5. Sound: Mathapelo and her mother discuss the business**

#### **6. Narrator:**

Mathapelo Ngaka amenunua shehena nzima ya mifuko ya plastiki ya rangi ya manjano, kuisafirisha hadi katika banda moja karibu na nyumba yake. Rinda lake jeupe linapeperusha na upepo, na huku akiwa amejifunga kitambara kichwani, anajaribu kupakua shehena hiyo ya mifuko ya plastiki katika chumba hicho kidogo karibu na nyumba yake. Ndani ya chumba hicho kumejaa mifuko ya plastiki na wanasesere wa kila aina. Vitu hivi vyote vya sanaa hukusanywa na Wanawake kutoka hapa kijiji cha Kayelitsha anaeleza Mathapelo. Nyumba ya Mamake inatumika kama kituo cha sanaa hiyo, huku pembe moja ya nyumba hiyo ikitumika kama eneo la kutoa mafunzo kwa kinamama.

### **7. Mathapelo:**

“Huwa tunawapa wasanii vifaa hivi vya sanaa bila malipo mfano shanga ....tunawapa bila malipo! Hapa kina Mama wanaotengeneza vitu vya sanaa hufanya kazi wakiwa majumbani mwao ili waweza kuendeleo na majukumu yao kama walezi wa nyumbani bila ya kutatizwa. Na pindi wanapokamilisha kutengeneza,wanaleta mali zao hapa. Sisi huchukua kila kitu wanacholeta na kuwalipa kabla ya kuviuza vitu hivyo.”

### **8. Narrator:**

Kwa Ufupi, hili ni shirika lisilo la faida kwa jina “Monkeybiz” lililoanzishwa na Mathapelo akishirikiana na msanii mmoja wa kutengeneza vitu vya kauri Shirley Fintz mnamo mwaka wa 2000. Lengo kubwa ilikuwa ni kubuni nafasi za kazi kwa Kinamama wanaoishi katika hali ya umaskini miongoni mwa jamii mbali na kufufua biashara ya shanga nchini humo.Mathapelo anacheka anapoulizwa iwapo biashara hiyo inauhusiano gani na mnyama Tumbili, kama jina linavyoashiria.

### **9. Mathapelo:**

“Tunasema sisi ni kama kundi la Tumbili tu, na kwamba “Monkeybiz” ni biashara ambayo huwezi kuichukulia kwa uzito.Tunaichukulia mzaha tu biashara hii, ni jambo la kuchekesha lakini imetuwezesha kuishi kama familia. Ndio sababu tukaamua kutumia jina hilo.

### **10. Narrator:**

Mathapelo, ambaye sasa ni mkurugenzi wa shirika hilo, anafurahia sana kueleza jinsi kampuni hiyo ilivyoanzishwa. Akiwa mtoto, alihudumu kama mfanyi kazi wa nyumbani kama mfanyanzi kabla ya kukutana na mnasihi wake na pia mfanyabiashara, Barbara Jackson.

### **11. Mathapelo:**

“Nilianza kufanya kazi ya ufinyanzi wa kauri mwaka wa 1998. Na ni hadi mwaka wa 1999 marehemu Barbara Jackson alipoona kazi yangu. Naweza kusema ilikuwa mipango ya mipango ya mungu tu kwani licha ya kwamba hakunifahamu mwanzoni, alitaka sana kukuza kipawa changu katika studio yake.

Wakati nikiwa katika studio yake, siku moja Mama alitengeneza bangili ya ushanga na kunipa nende kuwaonyesha wenzangu Studioni. Walishanga sana na kusema “Woow! Ni nzuri sana! Si kama zile zinazopatikana kila mahali mjini CapeTown.” Kisha wakanionyesha Mwanasesere mdogo ambaye walimununua wakati wa tamasha la maoneyesho mjini Grahamstown.

### **12. Narrator:**

Baadaye Mathapelo alirejea nyumbani na Mwanasesere huyo ambaye kumbe alikuwa ametengenezwa na Mamake. Watu wote katika studio hiyo walifurahishwa sana na utalaam huo, na huo ukawa mwanzo wa shughuli zetu za kutengeneza bidhaa hizi za “Monkeybiz” ambazo zinatambuliwa kote ulimwenguni.

### **13. Mathapelo:**

“Mamangu aliwafunza watu wengi sana sanaa hii. Lakini wengi wa washirika wapatao 450 wa shirika hili la Monkeybiz ni Wazee waliojifunza kazi ya kufuma shanga kutoka kwa mababu zao. Ni jambo la kufurahisha kuona ujuzi huu ukipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo maisha yangu yalibadilika kabisa wakati nilipokutana na Barbara Jackson.”

### **14. Sound: Mathapelo gives two women new commissions**

**15. Narrator:**

Mama huyo mwenye umri wa miaka 36 anatabasamu anapomkumbuka mnasihi wake aliyefariki mwaka wa 2010. Baada ya kupumua kidogo, anarejea ofisini mwake ili kuendelea na kazi.

**16: Sound: Shop at Monkeybiz**

**17: Narrator:**

Ofisi za shirika la Monkeybiz ziko katika Jengo la orofa kadhaa lenye rangi ya hudhurungi kwenye barabara nyembamba katika moja wapo ya mitaa ya kale mjini Cape Town.

Mathapelo Ngaka anaingia katika duka lililojaa vinyago vya wanyama na wanasesere. Baadhi ya vinyago hivi vimepangwa vizuri katika kabati la vioo lenya urefu unaokaribia kugusa paa la jingo hilo. Na vinyago wakubwa zaidi wamepanga mviringo kati kati ya duka hilo vikiangaliana kana kwamba viko katika kikao cha mazungumzo. Na cha kushangaza ni jinsi Mathapelo anavyofahamu vyema historia ya kila kinyago katika duka hilo.

**18: Mathapelo:**

“Chukua mfano wa kinyago hiki cha Mnyama. Kama unavyokiona kinapendeza sana. Kinyago hiki kimechongwa na Siziwe Lumkwana. (pronounced as written). Lumkwana ni msanii wa kuchonga vinyago na pia mwenye ujuzi wa kufuma shanga nzuri sana. Amekuwa akiishi maiasha magumu ya kudhulumiwa na Mumewe. Lakini tangu ajiunge na shirika hili la Monkeybis, maisha yake yamebadilika sana.”

**19: Narrator:**

Siziwe ni mmoja wa Wanawake 450 wanaofanya kazi katika shirika hili la “Monkeybiz”. Na Mathapelo Ngaka anafahamu vyema jinsi ya kutangamana nao. Yenye ni mchapa kazi na hajali muda utakaomchukua kufanya kazi anayoipenda zaidi. Kama mkurugenzi wa shirika hilo, yeye anapasa kufanya kazi kuanzia saa tatu hadi saa kumi na moja. Pia ni jukumu lake kuhakikisha kuwa mali iliyopo inatosheleza mahitaji ya Wateja. Na hii si kazi rahisi ikizingatiwa kwamba shirika hilo limewaahidi wasanii kwamba watanunua mali yote inayowasilisha katika shirika hilo.

**20: Mathapelo:**

“Ni jukumu kubwa. Kila wakati nafikiria , ‘Eh Mungu wangu wee ni wapi nitazitoa mali hizi?’ Na kila mara tunajaribu kuvumbua mbinu za kuongeza mali na kiwango cha uuzaji. Na zaidi watu wanaotengeneza mali hii pia wanaipenda kazi yao, wamejitolea kufanya kazi na kutengeneza mali nyingi sana kiasi cha kutupa wasi wasi mkubwa.”

**21: Narrator:**

Lakini hilo halimkoseshi usingizi mjasiriamali huyu chipukizi. Kinachompa msukumo ni Uchu wa kuifanya kazi hii na azma yake ndio inayowapa motisha watu wengine. Na kama shirika lisilozingatia faida, mapato yake hutumika kuimarish kiwango cha misha ya jamii wanamoishi. Mbali na miradi mingine inayotekelezwa na kina mama hao, shirika hilo pia linajishughulisha na mpango wa kuwasaidia wasanii walioambukizwa ugonjwa wa Ukimwi, kusimamia mkahawa unaouza supu ya kuku na kugawa vyakula. Na mradi wa hivi punde kabisa ulioanzishwa na shirika hili ni hazina ya kugharamia mipango ya mazishi kwa familia za Kina mama hao wanapopatwa na msiba.

**22: Sound: Mathapelo walks to her office**

**23: Narrator:**

Mathapelo anaondoka kupitia mlango wa nyumba wa duka hilo, kuelekea ofisini mwake kupitia chumba kimoja cha kuhifadhi mali ya shirika hilo. Ofisini, makaratasi yametapakaa kwenye meza yake vinyago ambavyo havijakamilika. Hapa tunakutana na Wanawake watatu wasaidizi wake wakiendelea na kazi yao ya komputa, kupokea simu na kujibu barua pepe. Mmoja wao ni Joan Krupp, afisa Meneja wa uhusiano na anfurahia sana kufanya kazi na Mathapelo.

**24: Joan:**

“Licha ya changamoto zinazotukumba, yeye hakati tama. Mathapelo hujizatiti kujiwamua kutoka hali yoyote ile. Na jambo la kufurahisha ni jinsi anavyoshirikiana na wenzake katika kubadilishana mawazo na ni Mtu aliyetayari kuwafunza wengune mambo mapya. Hilo ni jambo linalonifurahisha sana.”

**25: Narrator:**

Mathapelo Ngaka anatabasamu kusikia jinsi anavyosifiwa na wenzake, lakini hilo halimbabaishi, cha msingi ni kuimarisha zaidi biashara hiyo, na anaridhika na hatua aliyopiga kama mwanamke. Lakini pia anatambua mchango wa wanasihhi wake katika kukuza kipawa chake.



**26: Mathapelo:**

“Wao hunieleza kila kitu. Kwamba tunahitaji kutengeneza faida, ni vitu gani vinavyopasa kununuliwa au kuongezwa na gharama yake. Lazima utengeneze bidhaa ambazo zitawavutia wateja. Na hilo ni jambo la msingi linalozingatiwa na shirika la Monkeybiz, kutengeneza bidhaa zinazotosheleza mahitaji ya Mteja. Hatukuwa na pesa za kutosha lakini tulikuwa na ari ya kustawisha shirika hili la Monkeybiz na sasa linaendelea vyema kabisa.

**27: Sound: Mathapelos Office**

**28: Narrator:**

Wanzilishi wenza Barbara Jackson na Shirley Fintz walitumia akiba zao wenyewe kuanzisha shirika hili. Na mwaka wa pili biashara hiyo tayari ilikuwa inaweza kustawi na mtaji mzuriingawa kulikuwa na misaada kutoka kwa baadhi ya wahisani, mfano msanii mashuhuri nchini Afrika Kusini, Carol Boyes, ambaye alisaidia kutafuta soko la kimatifa kwa bidhaa za shirika hilo, zikiwemo shanga, vinyago na wanasesere mbali na kuwatengea chumba cha kuuza vinyago hivyo bila malipo. Na msada huo ndio uliwezesha kuitangza biashara ya shirika hili lya Monkeybiz katika soko la kimaafa bila ya gharama kubwa anasema Mathapelo.

**29: Mathapelo:**

“Naweza kusema kati ya asilimia 75 na 80 ya bidhaa za shirika hili zinazwa katika soko la kimataisa. Hapa nchini Afrika kusini wengi hawafahamu umuhimu au thamani ya vitu hivi vya sanaa. Kwa hivyo soko la kimataifa na hasa Marekani tuko na wateja wanaojua thamani ya bidhaa hizi na waridhishwa na kazi tunayofanya. Tuna bahati sana. Kwani kama hatungekuwa na soko hilo la kimataifa, sidhani kama tukekuwa bado tuko hapa”.

**30: Narrator:**

Soko la kimataifa, bidhaa za hali ya juu, usimamizi mzuri wa biashara, maongozi bora na maono ya kibiashara,ndio msingi wa ufanisi wa shirika hili la Monkeybiz lisilotafuta faida kutokana na shughuli zake na ambalo limepindukia kuwa mfano mzuri wa kiugwa na wafanyibiashara wengi. Na Mathapelo Ngaka huwa tayari kushauriana na Mtu yoyote mwenye anayetaka kuiga mfano wake kufika upeo mkubwa zaidi wa kibiashara.

**31: Mathapelo:**

“Ukiwa Mtu mwenye subira utafaulu maishani. Kila kitu kinahitaji subira. Kama singekuwa Mtu wa subira,na mwenye kukata tama haraka, singefika mahali nilipofika sasa. Ni lazima uwe na subira na pia Mtu mwenye kupenda kazi unayofanya,kwani hiyo ndio siri pekee ya ufanisi wa jambo lolote unalofanya.Hivyo lazima uwe mtu wa imani na kujituma pia”.

**Outro:**

Asante sana Mathapelo Ngaka na kwaheri. Umekuwa ukisikiliza hadithi ya Mathapelo, tukitumai kwamba umefurahia hadithi hii ya “Learning By Ear” Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu wajasiriamali wanaochangia pakubwa maendeleo ya namii wanamoishi barani Afrika. Mwandishi wetu alikuwa Leonie March. Endapo ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni yako usisite kutembelea mtandao wetu wa [www.dw.de/lbe](http://www.dw.de/lbe). Hadi wakati mwengine tutakapokutana tena kwa kipindi kingine cha Noa Bongo, Kwaheri kwa sasa.